**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA BUCHOSA**
*(Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya)*

Mkurugenzi Mtendaji Wilaya,
Halmashauri ya Wilaya ya Buchosa,
148 Br. ya Kayenze,
**33383 Nyehunge,**
**SENGEREMA, MWANZA.**

*Unapojibu tafadhari taja:*
**Kumb. Na. AB.03/117/01/VOL.II/11** Tarehe 28 Agosti, 2025

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI YA MKATABA

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Buchosa anapenda kuwatangazia watanzania wote wenye sifa nafasi za kazi ya Mkataba kwa nafasi zifuatazo;-

### 1.0 DEREVA DARAJA LA II - NAFASI TATU (03)

#### 1.1 Sifa za Muombaji

i. Awe amehitimu elimu ya kidato cha nne (IV) au cha sita (VI)
ii. Awe na leseni ya daraja la C au E ya kuendeshaji magari ambayo amefanyia kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja bila kusababisha ajali.
iii. Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji wa magari (Basic Driving Cource) yanayotolewa na chuo cha VETA, NIT au chuo kingine kinachotambulika na Serikali.

#### 1.2 Majukumu ya Kazi

i. kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari.
ii. Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi.
iii. Kufanya matengenezo madogomadogo ya gari.
iv. Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali
v. Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari na
vi. Kufanya usafi wa gari.

#### 1.3 Ngazi ya Mshahara

Kwa kuzingatia ngazi za mishahara ya Serikali yaani TGS B.

## 2.0 DEREVA WA BOTI DARAJA LA II – NAFASI NNE (04)

### 2.1 Sifa za Muombaji

i. Kuajjriwa waliohitimu mtihani wa kidato cha nne (IV) wenye ujuzi wa kuendesha na kutunza boti uliothibitishwa na chuo cha Dar es Saalam Marine Institute au chuo kingine chochote kinachotambuliwa na Serikali kwa muda usiopungua miaka miwili na waliofuzu mafunzo ya miezi sita ya uokoaji wa Maisha majini, kuogelea na kupanga watu au magari kwenye boti.

### 2.2 Majukumu ya kazi

i. Kufunga na kufungua Kamba za boti
ii. Kuchunga usalama wa abiria na magari yaliyomo ndani ya boti.
iii. Kupanga abiria au magari kwenye boti.
iv. Kuendesha na kuongoza boti.
v. Kutunza daftari za safari ya boti.
vi. Kuhakikisha kwamba injini ya boti ipo katika hali nzuri ya kufanya kazi.
vii. Kuangalia mafuta na vyombo vingine vya kufanyia kazi.

### 2.3 Ngazi ya Mshahara

Kwa kuzingatia ngazi za mishahara ya Serikali yaani TGOS A.

## 3.0 SIFA ZA JUMLA ZA WAOMBAJI:

i. Awe raia wa Tanzania.
ii. Awe na kitambulisho vya Taifa (NIDA)
iii. Awe amehitimu kitado cha Nne au cha sita
iv. Awe na umri wa Miaka 18 hadi 45
v. Mwombaji anatakiwa kuwa na wadhamini wawili wenye mali zisizohamishika katika maeneo wanakotoka.
vi. Mwombaji anatakiwa kuambatanisha picha mbili (pass port size) za rangi za hivi karibuni.
vii. Awe anajua kusoma na kuandika kwa ufasaha Lugha ya Kiingereza au Kiswahili.
viii. Awe mwaminifu,mwadilifu,na mwenye weledi.
ix. Awe hajawahi kupatikana na hatia kwa makosa ya jinai.
x. Mwombaji atakayekidhi sifa zinazotakiwa ataajiriwa na kupangwa kufanya kazi katika Halmashauri ya Buchosa.
xi. Barua ya maombi iwe na namba za simu na anuani ya kuaminika.
xii. Barua zote za maombi ziandikwe kwa mkono zikiwa na viambatanisho ambavyo ni nakala ya Cheti cha kidato cha nne au Kidato cha sita, Cheti cha Mafunzo ya fani husika pamona na wasifu wa muombaji (CV) na zitumwe kwa anwani ifuatayo;

**Mkurugenzi Mtendaji (W),**
**Halmashauri ya Wilaya ya Buchosa,**
**148 Br. ya Kayenze,**
**33383 Nyehunge,**
**SENGEREMA, MWANZA.**

Mwisho wa kupokea maombi ni Tarehe **13/09/2025** saa 9.30 Alasiri

**IMETOLEWA NA MKURUGENZI WA HALMSHAURI YA BUCHOSA**

Benson P.Mihayo
**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**
**BUCHOSA**

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
BUCHOSA

**NAKALA:**

✓ Mbao zote za matangazo Halmashauri ya wilaya ya Buchosa.